Jarida la Kiswahili Sanifu

# Usawiri wa Fatuma kama Kielelezo cha Mwanamke Shujaa wa Kiislamu katika Utenzi wa Fatuma

Simon Ekiru*

*Idara ya Elimu ya Ualimu, Chuo Kikuu Kishirikishi cha Turkana, Kenya.*

## IKISIRI

Makala hii inachunguza usawiri wa mhusika Fatuma kama kielelezo cha mwanamke shujaa wa Kiislamu katika Utenzi wa Fatuma. Madhumuni ya makala hii ni kubainisha namna mhusika Fatuma anavyowakilisha ushujaa wa mwanamke katika muktadha wa Kiislamu na jinsi anavyotumika kama mfano wa kuigwa na wanawake. Makala hii imetumia ufeministi wa Kiislamu kama kiunzi cha nadharia. Muundo wa kiuthamano unaojumuisha mbinu ya uhakiki wa matini ndiyo iliyotumika kukusanya na kuchanganua data ya utafiti. Data inayochanganuliwa inatokana na maelezo kutoka kwa Utenzi wa Fatuma. Matokeo ya makala hii yanaonyesha kuwa mhusika Fatuma amesawiriwa kuwa mtiifu kwa baba yake na mume wake, mwadilifu, mwaminifu katika ruwaza za dini ya Kiislamu, mwenye rajua ya kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake Waislamu siku ya kiyama, na jasiri. Kutokana na sifa zifa hizi, makala hii inadhukuru kuwa, mhusika Fatuma ni mfano wa mwanamke shujaa ambaye kwa kujitolea kwake katika dini, familia, na jamii, anaendeleza haki, usawa, na ustawi wa wanawake Waislamu. Aidha, mhusika Fatuma anawakilisha nafasi muhimu ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili, usawiri wake ukichangia katika kukuza uelewa wa mkabala wa ufeministi wa Kiislamu na kujenga mtazamo mpya kuhusu usawiri wa wanawake katika utenzi. Makala hii inatoa mchango muhimu katika utafiti wa fasihi ya Kiswahili kwa kuangazia mwingiliano kati ya fasihi, dini, na uana, na hivyo kubainisha namna vipengele hivi vinavyoshirikiana katika kujenga na kuimarisha taswira na nafasi ya wanawake katika jamii.

## KUHUSU MAKALA

*Maneno Muhimu:*
Haki,
Shujaa,
Ufeministi wa Kiislamu,
Usawa,
Utenzi.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 31 Machi 2026
Tarehe ya Kurekebishwa: 10 Aprili 2026
Tarehe ya Kukubalika: 26 Aprili 2026
Mtandaoni: 31 Julai 2026

## 1. Utangulizi

Tenzi za Kiswahili zimekuwa nyenzo muhimu za kuwasilisha taswira na mikabala ya kijamii katika mawanda ya uana na jinsia (Brown, 2022; Mwangi, 2021) Mifano ya tenzi hizi ni kama vile Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Hadija, Utenzi wa Mikidadi na Mayasa, na Utenzi wa Fatuma. Tenzi hizi zinaaminika kuwa miongoni mwa tenzi maarufu zilizo na wahusika wakuu wa kike ambao wanatumiwa na watunzi kuchora na kuwakilisha nafasi za wanawake katika jamii, hususan jamii ya Waswahili. Ikumbukwe kuwa Utenzi wa Mwanakupona ndio utenzi wa kwanza katika fasihi ya Kiswahili kutungwa na mwanamke (Mwangi, 2021). Utenzi wa Mikidadi na Mayasa vilevile ndio utenzi ulio na mwanamke jagina anayeitwa Mikidadi, ambaye ni mke wa shujaa Mayasa. Mikidadi licha ya kuwa mwanamke, ana ujasiri na nguvu nyingi pamoja na ujuzi wa kivita ambao unamwezesha kupigana na kuwashinda wanaume katika mapambano ya kivita (Burundi na wenzake, 2024). Hata hivyo, makala hii inazuumu kuchunguza Utenzi wa Fatuma kwa msingi kuwa, utenzi huu unaangazia kwa kina nafasi ya mwanamke wa Kiislamu katika jamii. Utenzi wa Fatuma ulitungwa na Binti Said Amin Bin Uthman aliyeishi kati ya mwaka 1800 na 1900 katika kisiwa cha Lamu, Pwani ya Kenya (Vutagwa, 2013). Utenzi huu unasimulia hadithi kuhusu ndoa ya Fatuma, binti yake Mtume Muhammad.

Katika utenzi huu, Fatuma anaonekana kama kielelezo cha mwanamke mwema, mwenye ujasiri wa kiroho, na maadili mema. Kichocheo cha maandalizi ya makala hii kinatokana na shauku ya kiusomi iliyomchochea mtafiti baada ya kusoma tafiti za Maina (2011), Vutagwa (2013), na Mutiso (2014) kuhusu Utenzi wa Fatuma. Ingawa tafiti hizi zinamwangazia mhusika Fatuma, tathmini ya mtafiti inabainisha kuwa hazijachunguza namna usawiri wake unavyompambanua kama kielelezo cha mwanamke shujaa wa Kiislamu. Hivyo basi, kuacha pengo la kiusomi ambalo makala hii inanuia kuliziba.

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: simonekiru@gmail.com

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Ekiru E. S. (2026). Usawiri wa Fatuma kama Kielelezo cha Mwanamke Shujaa wa Kiislamu katika Utenzi wa Fatuma. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(2), 1 – 9. https://doi.org/10.61889/h1g89q78.

© 2026 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

Kimsingi, makala hii inalenga kuchunguza jinsi utenzi huu unavyomsawiri Fatuma kama mhusika wa kipekee anayeunganisha nguvu ya kike na utakatifu wa kiimani ambazo ndizo nguzo za mwanamke shujaa wa Kiislamu. Makala hii hivyo basi, inanuia kutoa mchango katika mjadala unaoendelea kuhusu uana na jinsia katika fasihi ya Kiswahili. Makala hii imegawanywa katika sehemu zifauatazo: Mapitio ya maandishi, msingi wa kinadharia, mbinu za utafiti, matokeo ya utafiti, na hitimisho.

## 2. Mapitio ya Maandishi

Sehemu hii inadadavua dhana ya shujaa pamoja na udurusu wa tafiti zilizotangulia kuhusu Utenzi wa Fatuma. Udadavuzi huu unalenga kuelewa jinsi watafiti mbalimbali wanavyofasiri dhana ya shujaa katika miktadha tofauti ili kuweka msingi wa uelewa wa namna ilinavyojengwa ndani ya utenzi huu. Aidha, udurusu wa tafiti zilizotangulia kuhusu Utenzi wa Fatuma, unanuia kubainisha ufaafu wa tafiti zilizopo na pengo linalojitokeza ambalo makala hii inadhamiria kuliziba.

### 2.1. Dhana ya Shujaa

Katika tamaduni nyingi za Afrika, dhana ya shujaa imekuwa ikitumika kuashiria mtu wa kuigwa, mwenye ujasiri, aliyejitolea kwa hali na mali kwa ajili ya jamii, na mara nyingi kuhusishwa na mtu anyeshiriki katika mapambano na ukombozi wa kijamii, kiuchumi au kisiasa (Mazrui, 1978; Wa Thiong'o, 1981). Kwa mujibu wa Okpewho (1979) na Mulokozi na Madumulla (1998), shujaa ni mhusika mkuu katika utendi au kisakale, ambaye hutekeleza matendo makubwa ya kishujaa yanayoashiria ujasiri, nguvu, busara, na uadilifu. Hata hivyo, tafiti za hivi karibuni (Jansen van Vuuren, 2021; Nartey, 2022; Ombengi na Okemba, 2025; Oppong, Yeboah, Manu, na Issaka, 2023; Sam, 2025) zinaonyesha kuwa ufasiri wa dhana ya shujaa umebadilika kiasi kwamba haimrejelei tu mtu mwenye nguvu ya kivita au kimwili bali hurejelea mtu mwenye busara, anayewajibika na anayejitolea kutekeleza jambo fulani muhimu kwa ajili ya jamii, taifa, au ulimwengu wote. Nabea na wenzake (2017) wanatoa mifano ya mashujaa wanaotambulika barani Afrika kutokana na michango yao katika jamii. Wanasema hivi:

> "Hapa Afrika, pamekuwa na mashujaa wengi, na wengine wangali wanajenga ushujaa wao. Nchini Kenya, pamekuwa na mashujaa kama vile Dedan Kimathi, Wangari Maathai, Tecla Lorupe, David Rudisha n.k. Tanzania imeshuhudia mashujaa kama vile Kinjeketile Ngware, Mtemi Mkwawa Mwamnyika (Mkwawa wa Uhehe), Shabaan Robert n.k, Nchini Nigeria kumekuwa na mashujaa kama Ken Saro Wiwa, Chinua Achebe, Wole Soyinka, Nwankwo Kanu, Tarbo West, Sunday Oliseh, Augustine Azuka Okocha (Jay-Jay), ilhali nchini Ghana pamekuwa na mashujaa kama vile Kwame Nkrumah, Abedi Pele, Michael Essien, na Tony Yeboah."
> (Nabea na wenzake, 2017 uk. 101)

Kutona na fasili zilizotolewa na wasomi tuliyowarejelea, ni bayana kuwa ufasiri wa dhana ya shujaa ni nyumbufu kwa sababu hutegemea muktadha husika. Hali hii inatokana na namna watu au jamii mbalimbali hutunuku watu taji za ushujaa wakizingatia misingi tofauti, hivi kwamba shujaa kwa mtu mmoja si lazima awe shujaa kwa mtu mwengine. Aidha, ni muhimu kutambua kuwa mashujaa huweza kutunukiwa, kuandikwa historia, au fasihi (Nabea, Mwangi, na Mayaka, 2017). Kwa ujumla, dhana ya shujaa hurejelea mtu ambaye ana ujasiri, hekima, anayepigania haki na ukombozi wa jamii yake, anayelinda maslahi ya jamii yake, anayewakilisha maadili, matumaini na nguvu za watu, au anayenawiri katika jambo fulani na kuiletea jamii, taifa, au ulimwengu mzima fahari fulani. Kwa hivyo, ni muhimu kutambua kuwa maana ya shujaa hupanuka na kubadilika kiwakati na kimkuktadha. Kimsingi, shujaa ni mtu wa kuigwa, kupigiwa mfano, au kielelezo katika jamii.

Katika makala hii, dhana ya shujaa imefasiriwa katika muktadha wa fasihi ya Kiafrika. Hii ni kwa sababu Utenzi wa Fatuma ambao ndio kiini cha makala hii ni wa Kiafrika. Utenzi huu ulitungwa kwa mkabala wa Kiafrika na Mwafrika (Mswahili) aliyeitwa Binti Said Amin Bin Uthman aliyeishi kati ya mwaka 1800 na 1900 katika kisiwa cha Lamu, Pwani ya Kenya (Vutagwa, 2013). Vilevile, kwa kuwa utenzi huu umejikita katika maudhui na falsafa ya dini ya Kiislamu, dhana ya shujaa imefasiriwa pia katika muktadha wa Kiislamu. Utafiti uliozaa makala hii umefanya hivi kwa kuegemea maoni ya wanazuoni wanaoshikilia mkabala wa ufeministi wa Kiislamu (Ahmed, 2000; Barlas, 2019; Mernissi, 1991; Wadud, 1999). Wanazuoni hawa wanajaribu kumzindua mwanamke wa Kiislamu kwa kumpa misingi na mikabala ya kujikomboa na kuwakomboa si tu wanawake pekee, bali hata wanaume katika jamii. Kwa hivyo, maana ya shujaa katika makala hii inajumisha ujasiri wa matendo, uzalendo katika jamii, kutetea imani, dini, na haki, kuhimiza utu na mshikamano, kuchangia katika mabadiliko ya kijamii, kiungozi, na kiuchumi, kuwa kilelelezo na mfano bora wa kuigwa katika jamii kwa kufumbata hulka kama vile: Huruma, ujasiri, upole, urembo, elimu, subira, na unyenyekevu.

### 2.2. Tafiti za Awali Kuhusu Utenzi wa Fatuma

Katika utafiti wa tenzi za kale za Kiswahili, Utenzi wa Fatuma umebaki kuwa mojawapo ya tungo ambazo hazijapewa uzito unaostahiki katika tafiti za kiakademia. Tafiti zilizopo bado ni chache na hazijajikita kwa kina katika kuhakiki maudhui, mtindo, na falsafa zilizo ndani yake. Hali hii yamkini inachangiwa na ukweli kwamba utenzi huu uliandikwa kwa hati ya Kiarabu (Ajami) katika lahaja ya Kiamu cha kale, jambo linalowaletea changamoto watafiti wengi wa kisasa ambao aghalabu hukumbana na ugumu wa kusoma na kufasiri maandishi ya aina hiyo. Aidha, ukosefu wa wataalamu walio na umilisi na umahiri katika lahaja za kale za Kiswahili

umechangia kwa kiasi kikubwa kudhoofisha juhudi za kitaaluma katika utafiti wa utenzi huu.

Hata hivyo, mchango wa wataalamu wa kigeni, hususan Ernst Damman, hauwezi kupuuzwa. Ni Damman ndiye aliyefanikisha ukusanyaji, utafsiri, na uhifadhi wa kimaandishi wa Utenzi wa Fatuma, hivyo kuupa mwonekano wa kiakademia (Maina, 2011). Bila juhudi zake, huenda utenzi huu adimu japo adhimu ungepotea katika kumbukumbu za historia ya fasihi ya Kiswahili. Juhudi zake pamoja na wataalamu wengine wa kigeni zilifungua milango kwa watafiti wa baadaye kuutambua utenzi huu kama nyenzo muhimu katika kuelewa nafasi ya wanawake, ujumi wa kifani, na falsafa katika utunzi wa mashairi ya jadi ya Kiswahili (Vierke, 2017).

Wataalamu wengine wa kigeni waliyochangia pia katika maendeleo ya tenzi na mashairi ya jadi ya Kiswahili ni pamoja na J. W. T. Allen, Jan Knappert, na Alice Werner. Wataalamu hawa wamechangia pakubwa katika kuhifadhi na kuchambua tenzi nyingine mashuhuri kama Utenzi wa Inkishafi, Utenzi wa Hamziya, Utenzi ya Mikidadi na Mayasa, na Utenzi wa Mwanakupona. Kupitia juhudi zao za ukusanyaji, ufasiri, na uchambuzi wa kihistoria na kimitindo, wameweka msingi imara wa tafiti za kifasihi zinazohusu tenzi za Kiswahili. Kwa hivyo, tafiti za sasa kuhusu Utenzi wa Fatuma zinajitokeza kama juhudi za kujaza pengo la kihistoria na kitaaluma lililoachwa na tafiti za awali, huku zikijikita katika kuchunguza utenzi huu kwa mtazamo wa kisasa na wa Kiafrika. Utafiti uliozaa makala hii umebaini kuwa hadi kufikia sasa, tafiti zilizohakiki Utenzi wa Fatuma ni kama vile: Maina (2011), Vutagwa (2013), na Mutiso (2014).

Utafiti wa Maina (2011) unachunguza upembezwaji wa mwanamke kama udokezi wa nafasi yake katika Utenzi wa Fatuma. Kwa kuegemea nadharia ya ufeminsiti wa Kirasimi na mkabala wa ubabedume, matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa Fatuma hahusishwi katika maamuzi yoyote katika utenzi mzima kwa sababu ni mwanamke. Utafiti wa Maina (2011) ni afiki katika makala hii kwa sababu ndio uliompa mtafiti aliyeandika makala hii mshawasha, msingi wa kufasiri, na kuchambua Utenzi wa Fatuma. Hata hivyo, utafiti wa Maina (keshatajwa) unatofautiana na makala hii kwa sababu unachunguza namna mwanamke anavyopembezwa katika Utenzi wa Fatuma ilhali makala hii inachunguza namna Fatuma anavyowajibishwa na mtunzi kwa kusawiriwa kama kielelezo cha mwanamke shujaa wa Kiislamu. Aidha, utafiti wa Maina (keshatajwa) unaegemea nadharia ya Ufeminsti wa Kirasimi ilhali makala hii imejikita katika nadharia ya ufeministi wa Kiislamu.

Utafiti wa Vutagwa (2013) unashughulikia sifa za kiuhalisiajabu na umuhimu wake katika Utenzi wa Fatuma. Kwa kuegemea nadharia ya Uhalisiajabu, matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa matukio ya kiajabuajabu yanabainika katika Utenzi wa Fatuma. Vutagwa (keshatajwa) anadai kuwa matukio haya ya kiajabu yanaweza kukuza na kujenga imani dhabiti ya kidini miongoni mwa Waislamu. Utafiti huu ulimfaa mtafiti katika maandalizi ya makala hii kwa sababu unapambanua baadhi ya sifa za kipekee za Fatuma ambazo ndizo msingi wa uchanganuzi katika makala hii. Hata hivyo, utafiti wa Vutagwa (keshatajwa) unatofautiana na makala hii kwa sababu unachunguza matukio ya kiuhalisia-ajabu katika Utenzi wa Fatuma na kufafanua umuhimu wake ilhali makala hii inachunguza namna mwandishi anavyomsawiri Fatuma kama kielelezo cha mwanamke shujaa wa Kiislamu. Aidha, utafiti wa Vutagwa (keshatajwa) umejikita katika nadharia ya Uhalisiajabu ilhali makala hii imejikita katika nadharia ya ufeministi wa Kiislamu.

Utafiti mwingine unaoangazia Utenzi wa Fatuma ni utafiti uliofanywa na Mutiso (2014). Katika utafiti huu, Mutiso (keshatajwa) anashughulikia sitiari za nambari zinazodhihirika katika Utenzi wa Fatuma. Nambari zinazotumika kisitiari na mwandishi ni 1, 4, 7, na 1000. Mutiso (keshatajwa) anapambanua namna mwandishi anavyotumia nambari hizi kisitiari ili kuleta ujumi na hali kadhalika kusawiri matukio muhimu ya kiajabu na maudhui kuu katika Utenzi wa Fatuma. Utafiti huu ulimfaa mtafiti katika maandalizi ya makala hii kwa sababu baadhi ya matukio yanayohusisha nambari hizi za kisitiari yanazingira na kujenga uhusika wa Fatuma katika utenzi huu. Matukio haya ndiyo yanayotusaidia kupambanua sifa za kipekee za Fatuma, zinazomfanya kutamalaki kama mhusika nguli anayedhihiri ujumi wa kimaumbile, ukuu wa kimaadili, utukufu, na ushujaa wa kiimani miongoni mwa sifa nyingine, zinazomfanya awe kipenzi cha Allah, Mtume Muhammad, na watu wengi katika pembe zote za dunia. Hata hivyo, utafiti wa Mutiso (keshatajwa) unatofautiana na makala hii kwa sababu unajikita tu katika upambanuzi wa sitiari za nambari zinazotumika kusawiri matukio katika utenzi huu ilihali utafiti huu unajikita katika upambanuzi wa uhusika wa Fatuma kama kielelezo cha mwanamke shujaa wa Kiislamu.

Kwa muhtasari, udurusu wa tafiti za awali umebainisha kuwa Utenzi wa Fatuma umeshuhudia tafiti chache za kitaalamu katika fasihi ya Kiswahili. Pili, umeonyesha kuwa tafiti za awali hazikushughulikia usawiri wa Fatuma kama kielelezo cha mwanamke shujaa wa Kiislamu katika Utenzi wa Fatuma. Hivyo basi, makala hii inaziba mwanya uliowachwa kwa kupambanua namna mwandishi anavyomsawiri Fatuma kuwa kielelezo na mwanamke shujaa wa Kiislamu. Makala hii vilevile inaonyesha namna nadharia ya ufeministi wa Kiislamu inavyoweza kutumika kama mkabala faafu wa kuuhakiki wa Utenzi wa Fatuma.

### 2.3. Kiunzi cha Nadharia

Makala hii imejikta katika nadharia ya ufeministi wa Kiislamu iliyoasisiwa na kuendelezwa na wanazuoni wa Kiislamu kama vile Ahmed (2000, 2021), Alwani (2009), Barlas (2019), Dalaman (2021), Khan (2022), Mernissi (1991, 2022), na Wadud (1999). Nadharia hii ni mkabala wa kiuana unaolenga kuonyesha kwamba wanawake na wanaume wana nafasi na hadhi sawa ndani ya Uislamu. Tofauti na ufeministi wa Kimagharibi, ambao aghalabu huhusisha ukombozi wa wanawake kwa kujitenga na dini

au kuasi mifumo ya kitamaduni inayoegemea uumeni, ufeministi wa Kiislamu unasisitiza ukombozi wa mwanamke kupitia maandiko matakatifu ya Kurani, Sunna, na misingi ya sheria za Kiislamu. Nadharia hii inanuia kurekebisha taswira dumifu za uana zilizojengeka kihistoria, ambazo zimekuwa zikidumaza nafasi ya mwanamke katika jamii za Kiislamu.

Kwa msingi wa Kurani na Sunna, Uislamu unasisitiza kwamba wanawake hawakupangiwa kuwa wanyonge au wasio na mamlaka, bali washirika madhubuti katika jamii za Kiislamu. Nadharia hii inatetea heshima, elimu, na mamlaka ya kijamii kwa wanawake, ikionyesha kwamba Uislamu wa kweli haujamnyima mwanamke haki hizi. Badala yake, unamtambua mwanamke kama nguzo muhimu ya kijamii, kidini, na kimaadili katika ujenzi wa jamii za Kiislamu.Nadharia hii ina mihimili ifuatayo:

i. Usawa wa kiroho
ii. Ufasiri sahihi wa Kurani na Sunna
iii. Ukombozi kupitia imani
iv. Uadilifu wa kijamii na kimaadili
v. Kupinga mfumo dume wa kitamaduni

Katika makala hii nadharia ya ufeministi wa Kiislamu ni faafu kwa sababu inasaidia kuelewa nafasi ya mwanamke wa Kiislamu katika fasihi ya Kiswahili. Kupitia mihimili ambayo tumeiorodhesha katika makala hii, ufeministi wa Kiislamu ulimwezesha mtafiti kupambanua jinsi mhusika Fatuma katika Utenzi wa Fatuma alivyo kielelezo cha usawa wa kijinsia, ujasiri wa kiroho, ukombozi kupitia imani, na maadili mema.

## 3. Mbinu za Utafiti

Utafiti uliozaa makala hii ulifanywa maktabani kwa kutumia muundo wa kiuthamano wa uchanganuzi matini (DeMarrais na wenzake, 2024). Utenzi wa Fatuma uliotungwa na Binti Said Amin Bin Uthman ndio uliohakikiwa na kufanywa msingi wa data katika makala hii. Utenzi huu ulisampuliwa kimakusudi ili kukidhi madhumuni ya makala hii. Makala hii inalenga kupambanua namna mwandishi anamvyotumia mhusika Fatuma kuunda na kuchora taswira ya mwanamke shujaa wa Kiislamu. Nadharia ya ufeminsti wa Kiislamu imetumika kama kiunzi cha nadharia na vilevile katika uchanganuzi wa data husika. Data inayochanganuliwa inatokana na maelezo kutoka kwa Utenzi wa Fatuma. Mswada wa Dammann (1940) wa Utenzi wa Fatuma uliowasilishwa mwaka 1940, katika semina ya Chuo Kikuu cha Hamburg nchini Ujerumani, ndio uliotumika katika utafiti na maandilizi ya makala hii. Mswada wa Damman umetumika kwa sababu Damman ndiye mtafiti aliyehusika katika ukusanyaji, uhariri, na utafsiri wa Utenzi wa Fatuma pamoja na tenzi nyingine kama vile: Utenzi wa Yusuf, Utenzi wa Ayubu, na kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili zilizohifadhiwa kwa hati za Kiarabu (Ajami). Kwa kuwa Utenzi wa Fatuma umeandikwa katika mtazamo wa dini ya Kiislamu, makala hii vilevile ilidurusu vitabu vya Kiislamu vilivyosaidia kuelewa na kufasiri baadhi ya matukio yanayomzingira Fatuma.

## 4. Matokeo ya Utafiti na Mjadala

Sehemu hii inawasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Sehemu hii imegawanywa katika mada kuu zifuatazo: utiifu wa Fatuma kwa baba na mume, uadilifu wa Fatuma, uaminifu wa Fatuma katika ruwaza za dini ya Kiislamu, ombi la Fatuma kuwa mwombezi na mtetezi wa Wanawake wa Waislamu, na ujasiri wa Fatuma. Mada hizi kwa pamoja zinafafanua nafasi ya mhusika Fatuma kama kielelezo cha mwanamke shujaa ndani ya muktadha wa kidini na kijamii.

### 4.1. Utiifu wa Fatuma kwa Baba na Mume wake

Utiifu wa Fatuma kwa baba yake, Mtume Muhammad, na mume wake, Ali Talib, ni sifa muhimu ambazo zinamfanya kuwa mfano wa mwanamke shujaa wa Kiislamu, hasa katika mkabala wa ufeministi wa Kiislamu. Ufeministi wa Kiislamu unasisitiza usawa, haki, na uhuru wa wanawake, huku ukizingatia muktadha wa kimaadili na kidini (Barlas, 2019). Utiifu wa Fatuma, katika muktadha huu, hauonyeshi unyenyekevu wa kupuuzilia mbali haki au utu wa mwanamke, bali ni ishara ya kuheshimu nafasi za kimaadili na kidini katika jamii na familia ya Kiislamu.

Kwanza, utiifu wa Fatuma kwa baba yake, unaonyesha mfano wa mwanamke Mwislamu aliye na heshima kwa wazazi kama inavyosisitizwa na dini ya Kiislamu. Mtunzi anaeleza kuwa Fatuma alimtii na kumpenda baba yake, Mtume Muhammad. Tangu utotoni mwake hakukaidi amri za baba yake. Fatuma anaendeleza utiifu huu kwa Mtume Muhammad, kwa kumtambua na kumheshimu kama kiongozi wa dini ya Uislamu. Mtunzi anadokeza kuwa, Fatuma aliyafuata mafundisho na maelekezo ya baba yake kwa heshima bila pingamizi. Fatuma anafumbata dini ya Uislamu iliyoanzishwa na baba, akiwa bado mtoto mchanga kama ishara ya heshima na utiifu kwake. Haya yanadhihirika anapojishughulisha na mambo kama vile kwenda msikitini, kusali, na kujisitiri nyumbani. Haya ndiyo baadhi ya mambo aliyohimiza baba yake, Mtume Muhammad kuwa nguzo bora kwa mwanamke Mwislamu. Hulka hii ya Fatuma inabainishwa na mtunzi katika ubeti huu:

> Endapao msikitini,
> Kisa kusali Amini,
> Arudiapo nyumbani,
> Ali kimlingania (ubt. 98).

Utiifu wa Fatuma kama inavyodhihirika katika utenzi huu umejengwa katika mapenzi na heshima kwa Mungu, baba, na mume wake, na wala si kwa kuonyesha udhaifu au kupoteza nafasi yake kama mwanamke mwenye nguvu na uwezo.

Pili, utiifu wa Fatuma kwa mume wake, Ali, unadhihirisha picha ya mwanamke anayeishi katika mfumo wa ndoa ya Kiislamu, ambapo uhusiano wa mke na mume unapaswa kuwa wa ushirikiano, kuheshimiana, na kusaidiana. Katika mfumo huu, Fatuma anaonyesha wazi kuwa utiifu kwa mume wake si kupoteza haki zake au hadhi yake, bali ni mkakati wa kujenga ustawi na usalama katika ndoa, familia, na jamii yake. Katika utenzi huu, Fatuma hapingi wala kupuuza maamuzi na juhudi za mume wake kuendesha familia. Mtunzi anatueleza kuwa baada ya harusi yao, Fatuma na Ali wanajikuta katika hali ngumu ambapo hawana chakula katika nyumba yao (ubt. 334). Ali anaamua kwenda Shamu kutafuta kibarua ili apate pesa za kununua chakula (ubt.336). Fatuma hampingi bali anamwuunga mkono na kuridhia maamuzi hayo. Ali anafunga safari kwenda Shamu na kumwachia Fatuma jukumu la kulinda boma lao, wajibu anaoutekeleza kikamilfu na kwa heshima hadi Ali anaporejea na kulipata boma lao liko salama. Akiwa kule Shamu, Ali anapata kazi ambayo analipwa ujima wa peni tatu (ubt. 342). Anafunga tena safari kurudi Madina kwa mke wake Fatuma (ubt. 343). Akiwa njiani anakutana na maskini watatu ambao wanaomwomba msaada, anawahurumia na kuwapa pesa zote na kusalia bila chochote (ubt. 347-371). Anapoendelea na Safari, anakutana na kijana na ngamia anayeridhia kumwuuzia ngamia kwa deni (ubt. 366-370). Baadaye, anakutana na mwarabu anayenunua ngamia hiyo kwa dinari nyingi sana (ubt. 377-383). Pesa hizi ndizo Ali anazoamua kutumia katika maandalizi ya sherehe ya harusi yao.

Fatuma hapingi wala kutofautiana na maamuzi ya Ali. Anamruhusu kufanya hivyo kwa kuwa anaamini kwamba ni wajibu wa mwanamke wa Kiislamu kumheshimu mume wake ambaye ndiye kiongozi wa familia. Hata baada ya sherehe, Fatuma anaendelea kuheshimu maamuzi ya Ali hususan anapokata shauri kuwapa maskini pesa zake zote kama ishara ya zaka kwa wasiyojiweza katika jamii (ubt. 409). Katika muktadha wa ufeministi wa Kiislamu, hii inaonyesha maelewano ya kiuana na wadhifa wa wanawake katika ujenzi wa jamii. Wanawake wanasawiriwa kuwa washirika na wasaidizi muhimu kwa wanaume katika ujenzi wa familia thabiti yenye misingi yake katika heshima na ushirikiano (Ahmed, 2021; Dalaman, 2021). Hali hii inawasaidia kuepuka migogoro hivyo basi kutoa nafasi ya kila mmoja wao kuchangia na kutekeleza majukumu yake katika ndoa.

Kwa hivyo, utiifu wa Fatuma kwa baba yake na mume wake si kwa sababu ya shuruti za taswira dumifu za kiuana, bali ni utashi wa kudumisha maadili ya Kiislamu kwa kuzingatia heshima na uhusiano mzuri katika ndoa. Kwa kuegemea mtazamo wa ufeministi wa Kiislamu, Fatuma anajitokeza kama mwanamke mwenye nguvu na msimamo thabiti, ambaye anasimama kwa imani na kushirikiana na mwanamume katika ujenzi wa familia bora yenye misingi ya heshima, ushirikiano, na maelewano (Dalaman, 2021). Katika Kurani, kuna aya kadhaa zinazozungumzia kuhusu uhusiano wa kiutu na kiheshima kati ya wanawake na wanaume, na jinsi mume na mke wanavyopaswa kuhusiana. Mojawapo ya aya inayoangazia suala la utiifu katika ndoa na familia ni Surah An-Nisa (4:34):

> "Wanaume ni walinzi wa wanawake kwa sababu ya kile alichokupa Allah mmoja kuliko mwingine, na kwa sababu ya kile wanachotumia kutoka mali zao. Basi, wenye wema kutoka kwao ni wale wanaotekeleza majukumu yao kwa uaminifu na kwa heshima, na wale wanaojisalimisha kwa ushirikiano na kutii."

Aya hii inaonyesha wajibu wa kiuana katika familia za Kiislamu, ambapo mume anahusishwa na jukumu la uongozi na ulinzi kwa familia, huku mke akiwajibishwa kama mtu anayepaswa kuwa na heshima, ushirikiano, na utiifu kwa mume wake. Hata hivyo, jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba, katika muktadha wa ufeministi wa Kiislamu, aya hii haionyeshi udhaifu wa mwanamke mbele ya mwanamume, bali inathibitisha dhamira ya kumlinda na kumheshimu kama sehemu ya uhusiano wa usawa na haki, huku kila upande ukiwa na wajibu wake katika ujenzi wa ndoa na familia.

Ni kutokana na heshima ya Fatuma ndipo mume wake pamoja na baba yake wanaibuka kumpenda na kumthamini. Mtunzi anaeleza kuwa Ali alimwomba Allah ampe uwezo wa kumposa Fatuma kwa kuwa alimpenda na kumthamini (ubt. 104-107). Aidha, mtunzi anadokeza kuwa Mtume Muhammad alimpenda Fatuma kwa dhati ya moyo wake. Mtume Muhammad anaporejea nyumbani baada ya kutoka msikitini, analakiwa na kukumbatiwa na Fatuma. Mtunzi anasema hivi:

> Endapo alikimwita:
> “Nilia, ewe nyota”
> Fatuma akayivuta,
> mbeleze akimwemea (ubt. 99).

Fatuma anasawiriwa kama kipenzi cha baba yake. Upendo huu unamfanya mtume kumwombea Fatuma msamaha kwa Mungu. Kimsingi, matokeo haya yanaonyesha kuwa heshima ni mmojawapo wa nguzo muhimu katika kumjenga mwanamke shujaa wa Kiisalamu anayependwa na kuthaminiwa. Katika muktadha wa familia za Kiislamu, utiifu wa Fatuma kwa baba yake na mume wake unaweza kufasiriwa kama nguvu na uwezo wa mwanamke kukuza umoja wa kifamilia na mahusiano mazuri katika ndoa. Hizi ni nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii zenye usawa, upendo, na heshima.

### 4.2. Uadilifu wa Fatuma

Uadilifu wa Fatuma unamsawiri kuwa mwanamke shujaa wa Kiislamu kwa kuwa unajenga taswira ya mwanamke anayefanya maamuzi yake kwa misingi ya haki, uaminifu, na usawa, sifa ambazo ni msingi wa

ufeministi wa Kiislamu (Ahmed, 2000). Katika ufeministi wa Kiislamu, uadilifu unahusisha kudumisha haki na kuzingatia maadili ya kiuana ambayo yanajali usawa na heshima ya watu wote katika jamii. Kwa hivyo, uadilifu wa Fatuma unamfanya kuwa mfano wa mwanamke ambaye anatambua wadhifa wake na kuonyesha dhamira ya kulinda haki zake na za wengine katika jamii.

Mtunzi anadokeza kuwa Fatuma alikua bikira hadi alipoolewa na Ali (ubt. 94-96), hali inayothibitisha uadilifu wake katika maisha ya kijinsia na kiuana. Katika muktadha wa Kiislamu, Fatuma ni mfano wa wasichana wa Waislamu wanaoishi kwa heshima na kudumisha maadili na ustawi wa jamii. Kwa mujibu wa Ahmed (2000), ubikira wa Fatuma unaashiria uzingatifu wa maadili ya Kiislamu ambayo yamejikita katika usafi wa kimwili na kiroho. Kwa hivyo, uadilifu wake haupo tu katika kutii sheria za dini, bali pia kuishi kwa utulivu na utimilifu wa kiroho, huku akidumisha heshima ya mwanamke katika jamii.

Aidha, Fatuma anapobalehe, hakimbilii ndoa wala mahusiano ya kimahaba yanayoweza kumvunjia heshima, yeye pamoja na baba yake (Mtume Muhammad). Anajiheshimu na kujilinda dhidi ya maovu yanayoweza kumponza kwa kwenda msikitini, kusali, na kukaa nyumbani huku akifuata miongozo ya baba yake. Mtunzi anadokeza kuwa Fatuma alifuata na kusubiri mwongozo wa baba yake, Mtume Mohammad, kuwa ni Mungu tu ndiye atakayemchagulia mume (ubt. 110).

Mtume Muhammad anapoletewa ujumbe kutoka peponi na malaika Jibrili kuwa Mungu amemteua Ali Talib kuwa mume wa Fatuma (ubt. 263-273), Mtume anafurahi na kumpasha Fatuma ujumbe huo (ubt. 284-292). Fatuma hakaidi ujumbe huo. Anakubali kuolewa na Ali (ubt. 293-294). Ali anapokwenda Shamu kutafuta kazi (ubt. 336), Fatuma anasalia Madina kulinda boma lao. Anaishi maisha ya utulivu na utimilifu hadi mume wake anaporejea nyumbani. Zaidi ya hayo, anayazingatia maamuzi ya mume wake ya kutoa mali yao yote kwa maskini kama zaka (ubt. 409).

Matendo haya ya Fatuma hayafasiriwi tu kama ada ya mwanamke wa Kiislamu kuishi kwa amri za mwanamume, bali ni sehemu ya ushirikiano wa kimaadili na kiroho kwa mume na baba (Mernissi, 1991). Aidha, unawakilisha mfano wa ushirikiano wa kimaadili na kidini katika ndoa na familia. Alwani (2009) anadai kuwa wanawake wa Kiislamu wanapotii kwa dhamira ya kiroho na kwa kuzingatia haki za wengine, wanakuwa na nafasi ya kuwa viongozi wa maadili katika familia na jamii. Fatuma anazingatia miongozo ya baba yake na mume wake ili kuhakikisha kuwa familia yake inaishi kulingana na maadili ya Kiislamu. Hii ni kwa sababu maadili ya Kiislamu ndiyo nguzo kuu ambayo kwayo, haki za wanawake na wanaume hujengwa.

Kimsingi, matokeo haya yanaonyesha kuwa uadilifu wa Fatuma unaakisi maadili ya Kiislamu kuhusu haki, usawa, na heshima, na huu ndio msingi wa ufeministi wa Kiislamu. Fatuma anadhihirishwa kuwa mwanamke shujaa kwa kuzingatia maadili na kuchukua jukumu la kulinda familia na jamii. Hii inamwezesha kujenga familia na jamii yenye usawa na haki katika misingi ya maadili.

### 4.3. Uaminifu wa Fatuma katika Ruwaza za Dini ya Kiislamu

Uaminifu wa Fatuma katika ruwaza za Dini ya Kiislamu unamsawiri kama mwanamke shujaa wa Kiislamu kwa sababu Fatuma anaishi maisha ya kidini kwa kufuata miongozo ya Kiislamu. Kwa mujibu wa ufeministi wa Kiislamu, uaminifu katika dini haujikiti tu katika suala la kutii, bali pia katika dhamira ya kujitolea ili kujenga jamii yenye haki na usawa, ambapo wanawake wanapata nafasi ya kuwa viongozi wa kidini, familia, na jamii (Ahmed, 2021). Katika utenzi huu, Fatuma anaonyesha kwamba uaminifu ni nguvu inayomjenga mwanamke kidini, kijamii, na kifamilia, bila kupoteza utu wake wala nafasi yake katika jamii. Mtunzi anaeleza jinsi maisha ya Fatuma yamejengwa katika ruwaza za dini ya Kiislamu. Mtunzi anasimulia kuwa Fatuma aliishi maisha ya kidini tangu utotoni mwake. Alikuwa bikira aliyefuata miongozo ya Kiislamu. Aliyaamini na kuyafuata mafundisho na miongozo ya Mtume Muhammad, ambaye ndiye mwanzilishi wa dini ya Uislamu. Katika Surah Al-Ahzab (33:21), Kurani inasema:

> "Hakika katika Mtume wa Allah mnapata mfano mzuri wa kuigwa..."

Aya hii inasisitiza kwamba Mtume Muhammad ni kielelezo bora cha kuigwa kwa Waislamu wote ulimwenguni. Hivyo basi, kwa kumwamini Mtume Muhammad na miongozo yake, Fatuma anakuwa mfano bora kwa wanawake Waislamu, wanaohimizwa kufuata miongozo ya Mtume Muhammad kwa uaminifu. Aidha, Fatuma alitekeleza miongozo ya Mtume Muhammad kwa kushiriki ibada kama vile kusali, kwenda msikitini, na kuishi kulingana na mafundisho ya Uislamu.

Katika ndoa yake na Ali, Fatuma anaonyesha mfano wa mke mwaminifu, akithamini ndoa kama sehemu ya Sunna ya Mtume Muhammad (ubt. 293-294). Hii inadhahirisha uaminifu wake katika dini ya Kiisalamu, kwani Uislamu unathamini ndoa iliyojengwa kwa ushirikiano baina ya mwanamke na mwanamume wake kutekeleza majukumu ya kifamilia kwa usawa na heshima. Mtunzi anadokeza kuwa, uaminifu huu wa Fatuma kwa mume wake ulijenga upendo baina yao ambapo walibarikiwa kuwapata watoto wawili, Hassan na Hussein (ubt. 410-411). Aidha, Mtunzi anaendelea kusema kuwa, Fatuma alimwamini Ali kiasi kwamba anampa wosia wa namna ambavyo angependa kuzikwa pindi siku yake ya kukutana na Muumba wake itakapotimia. Anamwomba Ali, kumzika akiwa amevaa

hirizi yake aliyopewa na Mungu ili atapofukuka siku ya kiyama, hirizi hiyo iwe kitambulisho kuwa yeye ndiye mwombezi na mtetezi wa wanawake wote Waislamu (ubt. 412-417).

Hali hii inaonyesha imani thabiti aliyonayo kwa Mungu, na dini ya Kiislamu kuhusu ufufuo na siku ya kiyama. Vilevile, inaonyesha imani aliyonayo kwa mume wake kiasi kwamba anamwachia ujumbe huu nyeti kuhusu kifo na maziko yake. Ali anaridhia kuwa atatekeleza matamanio ya mke wake Fatuma (ubt. 418). Mernissi (1991) anasema kuwa ndoa ni muungano wa ushirikiano na uaminifu, na katika hili, Fatuma anaonyesha mfano bora kwa wanawake wa Kiislamu na kuwahimiza kuwa, uaminifu wao katika ndoa unawawezesha kupata haki na kutimiziwa na matamanio yao.

Kwa muhtasari, matokeo haya yanaonyesha kuwa uaminifu wa Fatuma unamsawiri kuwa mwanamke shujaa wa Kiislamu. Fatuma hachorwi tu kama mwanamke anayekubali kutii, bali pia mwanamke anayeishi kulingana na miongozo ya kidini kwa dhati, huku akiishi maisha ya imani, haki, na usawa. Kurani na maoni ya wanazuoni kama Ahmed (2021) na Mernissi (2022) zinathibitisha kuwa uaminifu wa Fatuma haukuwa tu kwa mume au baba yake, bali ulijikita katika maisha ya kidini, kijamii, na familia, akiwa mfano wa kiongozi wa kiroho, mke mwaminifu, na mwanamke mwenye nguvu ya kubadilisha jamii.

### 4.4. Ombi la Fatuma kuwa Mwombezi na Mtetezi wa Wanawake wa Waislamu

Ombi la Fatuma kwa Mungu kumfanya awe mwombezi na mtetezi wa wanawake wote Waislamu siku ya kiyama linadhihirisha sifa ya uongozi, huruma, na dhamira ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii ya Kiislamu. Katika makabala wa ufeministi wa Kiislamu, ombi hili linaweza kufasiriwa kama juhudi na azimio la wanawake Waislamu kutetea na kupigania haki yao ndani ya imani na dini. Aidha, ombi hili linaonyesha kwamba wanawake wana haki na uwezo wa kuwa na sauti katika jamii, na wanastahili kutetewa na kupiganiwa haki zao, si tu katika dunia hii, bali pia akhera. Fatuma, kama kielelezo cha mwanamke wa Kiislamu mwenye ujasiri na uthabiti wa kiroho, anajua kuwa wema wa jamii ya Kiislamu hauwezi kupatikana bila kuwatetea wanawake, ambao mara nyingi wanakosa sauti au haki zao katika jamii.

Mtunzi anaeleza kuwa harusi ya Fatuma na Ali ilipokamilika peponi, Mungu anamtuma malaika Jibrili akiandamana na malaika elfu sabini (70,000) wapeleke ujumbe duniani (ubt. 262-273). Mungu anawapa mahari wampelekee Mtume Muhammad kwa niaba ya Ali, kwa ajili ya kumwoa binti yake Fatuma. Malaika wanampelekea Mtume Muhammad mahari yenye thamani isiyopatikana duniani. Mtume Muhammad anapokea ujumbe kwa furaha na kwenda kumpasha binti yake Fatuma (ubt. 284-292). Fatuma bila pingamizi kwa Mtume anakubali kuolewa kwa Ali lakini anakataa mahari (ubt. 295-296). Fatuma badala yake anamtuma Mtume Muhammad awaeleze malaika kuwa anaomba Mungu ampe kibali cha kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wote Waislamu siku ya kiyama ( ubt. 304-306). Malaika Jibrili anapokea ombi hilo na kumpelekea Mungu (ubt, 307). Ombi la Fatuma linakubaliwa na Mungu (ubt. 308). Mungu anajibu ombi hili kwa kumtuma tena malaika Jibrili duniani kumpelekea Fatuma aya, kuashiria kuwa yeye ndiye mwombezi na mtetezi wa wanawake wote Waislamu siku ya kiyama (ubt. 313-314). Fatuma anaifunga aya kwa uzi na kuivalia kama hirizi kwenye shingo lake (ubt. 316).

Ombi hili la Fatuma kwa hakika linamsawiri kama kielelezo cha kiongozi bora wa wanawake Waislamu. Fatuma anasawiriwa kama kiongozi aliye na dhamira ya kutetea na kupigania haki za wanawake Waislamu. Wafeministi wa Kiislamu, huamini kuwa uongozi hauhusu tu suala la mamlaka ya kisiasa au kijamii, bali pia nafasi ya kuleta mabadiliko katika jamii kupitia utetezi wa haki na usawa. Khan (2022) anasisitiza kwamba wanawake Waislamu, kama Fatuma, wanapaswa kuwa na nafasi ya kuwa viongozi wa kiroho na haki, na kwamba maombi ya Fatuma ni kielelezo cha udhihirisho wa nguvu na jukumu la wanawake katika jamii. Kwa hivyo, ombi la Fatuma kumtaka Allah amfanye kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake Waislamu siku ya kiyama linamaanisha kuwa, wanawake wanapaswa kuwa na sauti katika masuala ya kidini, kisiasa, kisheria, na kijamii, na kwamba wanatambuliwa kama sehemu muhimu katika jamii ya Kiislamu.

Aidha, ombi hili pia linahusiana na haki za wanawake katika muktadha wa Kiislamu. Ahmed (2021) anasisitiza kuwa wanawake wa Kiislamu wanastahili kutambuliwa na kuheshimiwa katika jamii, na kwamba wana haki ya kutetewa, hasa katika siku ya kiyama, ambapo kila mtu atahesabiwa kwa matendo yake. Fatuma anaona umuhimu wa kutetea wanawake, na ombi lake linaakisi mtindo wa maisha ya Waislamu kuwa ni jamii inayojali na kutekeleza haki za wanawake. Hivyo, kufanywa kwa Fatuma kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake Waislamu siku ya kiyama, kunaasharia nguvu walizonazo wanawake wa Waislamu kubadilisha hali zao.

Kwa hivyo, ombi la Fatuma kumtaka Allah kumfanya kuwa mtetezi wa wanawake Waislamu siku ya kiyama linamsawiri kuwa mwanamke shujaa wa Kiislamu kwa kuonyesha kuwa wanawake wanastahili kutetewa na kupigania haki zao, si tu katika dunia hii, bali hata akhera. Kupitia ombi hili, Fatuma anasisitiza nafasi muhimu ya wanawake katika jamii ya Kiislamu na umuhimu wa kuhakikisha haki zao zinatambuliwa na kuendelezwa.

### 4.5. Ujasiri wa Fatuma

Ujasiri wa Fatuma katika utenzi huu unamsawiri kuwa mwanamke shujaa wa Kiislamu. Kupitia matendo yake ya kijasiri anaonyesha uthabiti na dhamira ya kupigania haki za wanawake na kuwa mfano wa kiongozi wa kiroho na kijamii. Katika misingi ya ufeministi wa Kiislamu, ujasiri haujumuishi tu kukabiliana na changamoto, bali pia ni dhamira ya kuhakikisha kuwa kuna usawa na haki katika jamii (Ahmed, 2021; Mernissi, 2022). Aidha, ujasiri wa Fatuma, unatajwa mwanzoni mwa utenzi huu na mtunzi. Mtunzi anaeleza kuwa Mungu alipoumba ulimwengu, aliumba viumbe vinne vinne na katika kila vinne hivyo, akateua kimoja ambacho ni bora zaidi (ubt. 64-88).

Mtunzi anadai kuwa Mungu aliwaumba wanawake wanne jasiri. Wanawake hawa ni Hawa (mama wa ulimwengu mzima), Sarai (mke wa Nabii Ibrahim), Mariamu (mama wa Nabii Isa au Yesu), na Fatuma (binti wa Mtume Mohammad). Mtunzi anaisifia ujasiri wa Fatuma kwa kudai kuwa yeye ndiye mwanamke bora duniani na hata akhera, na ndiye ambaye amepewa kibali cha kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wote Waislamu siku ya kiyama. Ujasiri huu wa Fatuma unakuja kudhihirika baadaye katika utenzi huu pale ambapo Fatuma anapokataa mahari anayopwewa na Allah, badala yake kuomba awe mwombezi na mtetezi wa wanawake wote Waislamu siku ya kiyama. Hii ni ishara ya ujasiri na kujitolea kwake kwa ajili ya haki za wanawake, akijua kuwa wanawake wanahitaji kutetewa na kupiganiwa nafasi zao, si tu katika dunia hii bali hata akhera. Ujasiri huu unathibitisha kwamba wanawake wana nafasi ya kuwa viongozi wa kijinsia na kiuana, wakiwa na sauti katika masuala ya kidini na kijamii. Kwa hivyo, ujasiri wa Fatuma ni mfano wa nguvu ya kiroho na kijamii, inayozingatia usawa na haki kwa wanawake katika jamii ya Kiislamu.

## 5. Hitimisho

Kwa kuhitimisha, makala hii inaonyesha kwamba usawiri wa Fatuma katika Utenzi wa Fatuma unatoa taswira ya mwanamke shujaa wa Kiislamu mwenye sifa za kipekee, ikiwa ni pamoja na utiifu kwa baba yake na mume wake, uadilifu wake, uaminifu katika ruwaza za dini ya Kiislamu, rajua yake ya kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wote Waislamu, na pia ujasiri wake. Mtunzi anamtumia Fatuma kama kielelezo cha nguvu na imani thabiti kwa wanawake Waislamu. Aidha, kupitia uhusiano wa Fatuma na baba yake, Mtume Muhammad, pamoja na mume wake, Ali, mtunzi anaonyesha namna mwanamke anavyoweza kuwa wenzo wa kujenga umoja wa kifamilia ili kudumisha haki na ustawi wa jamii. Kwa hivyo, makala hii inatoa mchango muhimu kwa wanawake Waislamu, kwani tahakiki hii inaonyesha jinsi mtunzi anavyomsawiri Fatuma kuonyesha uwezo wa mwanamke Mwislamu kutumia nguvu na miongozo ya Uislamu kujikomboa na hata kuwakomboa wanawake wengine kwa kutetea nafasi na hadhi yao katika jamii. Kupitia uhusika wa Fatuma, wanawake Waislamu wanaweza kupata motisha na yamkini kupigania nafasi zao za kustawi na kujenga jamii zinazozingatia haki, usawa, na maadili. Kwa wanawake duniani kwa ujumla, Fatuma ni mfano wa wanawake wanaojitahidi kuleta mabadiliko katika jamii, kwa kutetea na kupigania hadhi na nafasi ya wanawake.

Mwisho, makala hii ni mchango muhimu katika kuendeleza utafiti kuhusu nafasi ya wanawake katika utenzi, hasa kwa kuzingatia kwamba utenzi, kama aina ya fasihi, umejikita katika usawiri wa mashujaa na hadithi za kihistoria. Makala hii pia inachangia katika upanuzi wa nadharia ya ufeministi wa Kiislamu katika fasihi ya Kiswahili, na kuleta mtazamo mpya kuhusu nafasi ya wanawake katika utanzu huu. Kimsingi, makala hii haichangii tu katika fasihi ya Kiswahili, bali pia inatoa msingi wa kujenga na kuimarisha mahusiano ya wanawake katika muktadha wa kisiasa na kihistoria, ikiangazia umuhimu wa kuwakilisha wanawake kama mashujaa wenye nguvu na hadhi.

## Marejeleo

Ahmed, L. (2021). Women and gender in Islam: Historical roots of a modern debate. New Haven, CT: Yale University Press.

Ahmed, S. M. (2000). Women and gender is Islam. The Ahfad Journal, 17(2), 61-63.

Alwani, Z. (2009). Family Relations: An Islamic Perspective. July, 2009 Arlington, TX USA, 33-65.

Barlas, A. (2019). Believing women in Islam: Unreading patriarchal interpretations of the Qur'an. Austin: University of Texas Press.

Brown, N. M. (2022). Swahili Poetry, Classical Tradition. In, Encyclopedia of African Religions and Philosophy (pp. 650-653). Dordrecht: Springer Netherlands.

Burundi, R. N., Mugambi, A., & M'Ngaruthi, T. K. (2024). Uhusika katika Fasihi Bulibuli ya Kiswahili: Mfano Kutoka Utenzi wa Mikidadi na Mayasa. https://scholar.google.com/scholar?hl=en&as_sdt=0%2C5&q=Burundi%2C+R.+N.%2C+Mugambi%2C+A.%2C+%26+M%E2%80%99Ngaruthi%2C+T.+K.+%282024%29.+Uhusika+katika+Fasihi+Bulibuli+ya+Kiswahili%3A+Mfano+Kutoka+Utenzi+wa+Mikidadi+na+Mayasa.&btnG=. Ilipakuliwa 23/12/2025.

Dalaman, Z. B. (2021). From secular Muslim feminisim to Islamic feminism (s) and new generation Islamic feminists in Egypt, Iran and Turkey. Border Crossing, 11(1), 77-91.

Dammann, E. (1940). Dichtungen in der Lamu-Mundart des Suaheli (Band 28). Hamburg: Friederichsen, de Gruyter & Co.

DeMarrais, K., Roulston, K., & Copple, J. (2024). Qualitative research design and methods: An introduction. Stylus Publishing, LLC.Mji?

Jansen van Vuuren, A. M. (2021). (Re) constructing the heroic narrative in four South African Anglo Boer War Films. Stilet: Tydskrif van die Afrikaanse Letterkundevereniging, 33(1), 31-51.

Khan, A. A. (2022). The Unforgettable Queens of Islam: Succession, Authority, Gender: By Shahla Haeri. New York: Cambridge University Press.

Maina, H. G. (2011). Upembezwaji wa Mwanamke Kama Udokezi wa Nafasi ya Mwanamke Katika Utenzi wa Fatuma (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Mazrui, A. A. (1981). Dual Zimbabwe: toward averting political schizophrenia. African Issues, 11(3-4), 5-12.

Meinhof, C. (1911). Die Dichtung der Afrikaner: hamburgische Vorträge (No. 43). Berliner Ev. Missions. Gesellschaft.

Mernissi, F. (1991). The veil and the male elite: A feminist interpretation of women's rights in Islam. Cambridge, MA: Perseus Books.

Mernissi, F. (2022). La Femme dans l'insconscient musulman. In, De la culture marocaine moderne (pp. 312-314). En toutes lettres.

Mulokozi, M.M na Madumulla, J. (1988). Mukwava wa Uhehe: Utangulizi na Uchambuzi. Dar es Salaam: DUP.

Mutiso, K. (2014). Number symbolism (nos. 1, 4, 7 and 1,000) in Swahili poetry: the case of Utenzi wa Fatumah. Kiswahili, 77(1), 132–148

Mwangi, E. M. (2021). Swahili literature. A companion to african literatures, 79-99.

Nabea, W., Mwangi J. N. na Mayaka, G. (2017). Matendo ya Wahusika Wakuu katika Tendi Teule za Kiswahili: Ushujaa au Uhayawani? Katika, Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja. uk. 101-111.

Nartey, M. (2022). Political Myth-making, Nationalist Resistance and Populist Performance: Examining Kwame Nkrumah's Construction and Promotion of the African Dream. Routledge https://scholar.google.com/scholar?hl=en&as_sdt=0,5&q=8.+Nartey,+M.+(2020).+kwame+nkrumah. Ilipakuliwa 23/12/2025.

Okpewho, I. (1979). The epic in Africa: Toward a poetics of the oral performance. Columbia University Press.

Okpewho, I. (1996). How Not to Treat African Folkore. Research in African Literatures 27 (3): 119–127.

Ombengi, N. E., & Okemba, L. C. (2025). A comparative Analysis of African Epic Hero Trait Depictions in the Epics of Fumo Liyongo, Mikidadi na Mayasa and Swifa ya Nguvumali. International Journal of Literature, Language and Linguistics 8(2), 130-152.

Oppong, P. S., Yeboah, P. A. O., Manu, J. G., & Issaka, C. A. (2023). The Heroine's Monomyth: A Study of Buchi Emecheta's Kehinde. NOBEL: Journal of Literature and Language Teaching, 14(2), 133-148.

Sam, C. A. (2025). Narrating Humanity to the African Child: Deconstructing the Hero Figure in Naana JES Opoku-Agyemang's Who told the Most Incredible Stories (Vols 1-5). Contemporary Journal of African Studies, 12(1), 1-20.

The Qur'an [Kiswahili version]. (n.d.). Islamhouse. https://islamhouse.com/sw/books/2804142/. Ilipakuliwa 26/12/2025.

Vierke, C. (2017). The Making of the 'Classical'Utenzi: a Consideration of the Early Editorial History of Tenzi in the 19th and 20th Century. Katika, Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja. Uk. 113-130.

Vutagwa, F. L. (2013). Sifa za kiuhalisiajabu na umuhimu wake katika utenzi wa mwana Fatuma (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Wa Thiong'o, N. (1981). Writers in Politics: Essays. Nairobi: East African Publishers.

Wadud, A. (1999). Qur'an and woman: Rereading the sacred text from a woman's perspective. Oxford: Oxford University Press.